# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dodoma***
***28 Juni, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewahimiza wananchi kutumia fursa ya mbolea ya bei nafuu inayozalishwa nchini kuongeza uzalishaji, akitaja uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha mbolea kama hatua muhimu ya kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa mbolea na kuongeza tija kwenye kilimo nchini.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kuzalisha mbolea cha ITRACOM Fertilizers Limited kilichopo Nala, jijini Dodoma, uzinduzi uliohudhuriwa pia na Rais wa Jamhuri ya Burundi, Mhe. Évariste Ndayishimiye.

Rais Dkt. Samia amesema kuwa sekta ya kilimo imeendelea kuteseka kutokana na utegemezi mkubwa wa mbolea kutoka nje, ambapo hadi asilimia 90 ya mbolea inayotumika barani Afrika huagizwa, hali inayochangia matumizi ya mbolea kuwa wastani wa chini ya kiwango kinachoshauriwa, na hivyo kuathiri uzalishaji.

Aidha, amesema kuwa uwepo wa kiwanda cha kuzalisha mbolea cha ITRACOM Fertilizers Limited chenye uwezo wa kuzalisha tani milioni moja kwa mwaka ni mkombozi mkubwa katika sekta ya kilimo.

Rais Dkt. Samia pia amesema ujenzi wa kiwanda hicho ni kielelezo cha jitihada za Serikali katika kukuza sekta ya kilimo kwa kuhamasisha uwekezaji, ambapo hadi sasa kiwanda hicho kimeajiri wafanyakazi 1,500, huku idadi hiyo ikitarajiwa kufikia lengo la kiwanda la kufikisha ajira 3,000.

Halikadhalika, ameeleza maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa Serikali wa ruzuku ya mbolea unaolenga kupunguza gharama kwa mkulima na kuongeza matumizi ya mbolea ya ndani, huku wakulima wengi zaidi wakitegemewa kunufaika na mbolea ya bei nafuu.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia amekitaka kiwanda hicho kuimarisha mfumo wa usambazaji wa mbolea hadi kwa wakulima wa vijijini, na kushirikiana na taasisi za utafiti wa kilimo pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa elimu kwa kwa wananchi juu ya matumizi bora ya mbolea.

Akieleza mafanikio ya uwekezaji huo mkubwa, Rais Dkt. Samia ameweka bayana uhusiano wa kimkakati kati ya Tanzania na Burundi, na kwamba nchi hizo zimeendelea kushirikiana kwa karibu kukuza biashara na kutekeleza miradi ya pamoja ikiwemo ujenzi reli ya SGR kutoka Uvinza hadi Musongati.

Kwa upande wake, pamoja na mambo mengine, Rais Évariste Ndayishimiye amepongeza uhusiano mzuri uliopo kati ya Burundi na Tanzania, na kuongeza kuwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na kampuni ya ITRACOM Fertilizers Limited ya Burundi katika Jiji la Dodoma unaashiria dhamira ya kukuza mshikamano uliopo baina ya nchi hizi mbili.

Akihutubia kwa lugha ya Kiswahili, Rais Ndayishimiye amesema kiwanda hicho kimeweka daraja lingine la mahusiano baina ya Burundi na Tanzania, na kuongeza kuwa kwa sasa Warundi wanakuja Tanzania kama wawekezaji, tofauti na zamani ambapo walikuwa wanakuja kama wakimbizi.

Aidha, Rais Ndayishimiye amesema uwepo wa kiwanda hicho utapunguza gharama za kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi, hivyo kuwaongezea wakulima uhakika wa kupata mbolea, na hivyo kuhakikisha usalama wa chakula barani Afrika.

Mapema leo kabla ya uzinduzi wa kiwanda, Rais Dkt. Samia amewaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni katika hafla iliyofanyika Ikulu Chwamwino.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

Viongozi walioapishwa ni pamoja na Wakuu wa Mikoa ya Kigoma, Iringa, Shinyanga, Mbeya, na Songwe, Katibu Mkuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Naibu Makatibu Wakuu wa wizara mbalimbali.

Rais Dkt. Samia amewaasa viongozi hao kuhakikisha usalama na amani ya nchi hasa katika kipindi cha kuelekea maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, kusimamia matumizi bora ya fedha za umma, kuongeza ukusanyaji mapato na kuhudumia wananchi kwa kuzingatia vipaumbele muhimu.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu